

# »Jinsi ya kutumia hatua nzuri za usalama shambani«

Usalama shambani unahusisha mbinu zote zinazotumika kabla na wakati wa kufuga wanyama ili kuboresha hali za ufugaji na kupunguza uwepo wa vimelea vya magonjwa.

Mlipuko wa magonjwa shambani huathiri matokeo ya kitaalam na kiuchumi. Hata hivyo, magonjwa haya yanaweza kudhibitiwa kwa ufanisi kwa kutekeleza hatua za usalama. Unapotumia viuatilifu, hakikisha kwamba unatumia dawa zenyе ufanisi ili kuua vimelea vya magonjwa.

## Hatua za usalama

Punguza uwasiliano kati ya wanyama wa kufugwa na wanyama porini kwa kuweka uzio kuzunguka shamba.

Pia dhibiti ufikiaji wa watu shambani, na hakikisha unaosha na kuua viini kwenye magari yanayoingia shambani ili kuzuia uchafuzi kutoka kwa vimelea vya nje.

Watu wanaoingia shambani wanapaswa kuoga na kuvaan nguo safi. Tenganisha wanyama wapya walionunuliwa kwa mwezi mmoja ili kuepuka kueneza vimelea vya magonjwa.

Tumia uhimilishaji bandia, na angalia shamba lilitolewa shahawa ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa ya sehemu za uzazi.

Pia ni muhimu kutenganisha wanyama kulingana na umri ili kuongeza upinzani kwa magonjwa.

Hakikisha unasafisha na kukausha banda ili kuondoa kuua vimelea vya magonjwa. Baada ya kusafisha, usitumie banda kufuga wanyama wapya kwa siku 7.

Hakikisha kwamba vifaa vinavyotumiwa lazima vimesafishwa. Weka nyavu kwenye banda ili kuzuia ndege wa porini wanaobeba

vimelea vya magonjwa.

Pia tekeleza mpango wa kudhibiti na kuondoa wadudu kwenye eneo, na usitumie mabaki ya jikoni bali tumia malisho kutoka kwa muuzaji anayeaminika.

Tia dawa kwenye maji ya kunywa ya wanyama, safisha mfumo wa usambazaji wa maji ili kuondoa vimelea vya magonjwa.

Hakikisha unachanja mifugo ili kuongeza kinga za wanyama dhidi ya virusi, tenganisha wanyama wagonjwa ili watibiwe ipaswavyo. Choma wanyama waliokufa, tibu samadi ili kuua vimelea vya magonjwa.